# Simba Sc yatoa tambo



## Mabadiliko tabia nchi ni muhimu...

fikrapevu @fikrapevu @fikrapevu


# BUSATI

Ukweli na Uhakika

Tovuti: www.busati.co.tz | ISSN 3456-3421 Toleo Na.14 Busati Jumanne Februari 4, 2025 Bei Tsh. 1,000 | Ksh. 100




### KUENDELEZA MEMA ALIYOANZISHA...

# Rais Dk. Samia mitano tena

- Watanzania wafurahishwa na kile anachofanya kwa sasa
- Waiona tanzania ilivyopiga hatua kubwa, wazidi kumchangia Fedha ya fomu
- Hii ni kuridhishwa na jitihada zake za kuipaisha nchi katika uchumi

> "Kwa hiyo huko asijitokeze mwingine anataka kumchukulua mama fomu, wana Chato tumechanga pesa ya kutosha Mama Samia kuchukua fomu, kwenye maombi ya kuiombea nchi wana Chato tumeshachanga," alisema Mwenyekiti wa Kamati ya Amani ya Wilaya, Sheikh Abdalah Aman Isimail.

## Utamaduni ni fursa ya kukuza utalii

# Mbolea ya Tanzania kuuzwa Uganda

NA MWANDISHI WETU


**WAZIRI wa Viwanda na Biashara Dkt. Selemani Jafo amesema fursa ya Tanzania kuuza mbolea inayotengenezwa na Kiwanda kinachozalisha mbolea asilia cha Intracom Fertilizer limited IFL nchini Uganda kutaongeza ajira, Pato la Taifa, kukuza uchumi na uhusiano wa kibiashara kati ya nchi hico mbili.**

Dkt. Jaffo aliyasema hay hivi karibuni, wakati Waziri Mkuu wa Uganda Robinah Nabbanjah alipotembelea kiwanda hicho na kuonyesha kuridhishwa na uwekezaji uliofanyika, ambapo kinazalisha mbolea asilia ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi pamoja na kulinda afya ya udongo.

Aidha, Waziri Jafo amesema kiwanda hicho kilichoanza kuzalisha mbolea tani 200000 kwa mwaka na kwa sasa kinauwezo wa kuzalisha tani 800,000 kwa mwaka na kinapanga kuongeza uzalishaji tani 1000,000 kwa mwaka kwa sasa kinauwezo wa kuzalisha mbolea kwa mahitaji ya ndani na nje ya nchi.

Aidha amefafanua kuwa uuzaji wa mbolea hiyo nchini Uganda ni moja ya utekelezaji wa makubaliana ya kufanya biashara ndani ya ncxhi za Afrika Mashariki na Mkataba wa Eneo huru la Biashara Afrika (AfCFTA)

Vilevile Dkt Jafo amefafanua kuwa Kiwanda hicho kinachotoa ajira ya moja kwa moja 827 kinazalisha aina kumi za mbolea ikiwemo FOMI Otesha, FOMI Kuzia, FOMI Nenepesha, CHOKAA Kilimo, FOMI Chai+, FOMI Chai++, FOMI Cans, FOMI Junia and FOMI Supa kitaongeza uzalishaji na ajira zaidi kitakapoendelea kupanua uzalishaji na kuongeza mauzo ya mbolea hizo ndani na nje ya nchi.



# Mapato yakusanywa hadi kuvuka lengo

NA ALBANO MIDELO, Songea

**Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, mkoani Ruvuma, imefanikiwa kukusanya mapato ya zaidi ya shilingi bilioni mbili sawa na asilimia 101 ya lengo.**

Taarifa hiyo imetolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Philemon Magesa, wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani cha kujadili utekelezaji wa shughuli za kamati za kudumu za Halmashauri kwa robo ya pili ya mwaka wa fedha 2024/2025.

Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, Haruna Mang'uli, amepongeza usimamizi mzuri wa mapato unaofanywa na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo.

Hata hivyo amewakumbusha wananchi kuhakikisha watoto wao waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wanaripoti katika shule walizopangiwa.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, Mheshimiwa Juma Pandu, amepongeza madiwani na watumishi wa halmashauri kwa juhudi zao zilizowezesha kuvuka malengo ya ukusanyaji wa mapato.

# Bunge latoa kauli kiwanda kufufuliwa

NA MWANDISHI WETU

**KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo imeipongeza Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) kwa utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati na Kielelezo ya Liganga Mchuchuma, Magadi soda na ufufuaji wa Kiwanda cha KMTC Manufacturing Limited yenye maslahi makubwa katika ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini.**

Hayo yamesemwa na Mwenyekiti wa Kamati Deodatus Mwanyika wakati wa Waziri wa Viwanda na Biashara akiwasilisha Taarifa ya Utendaji wa Kiwanda cha KMTC Manufacturing Limited kilichosajiliwa Kampuni Tanzu ya NDC mwezi Machi, 2023 kilichojulikana kama Kilimanjaro Machine Tools Company (KMTC) ili kufanya kiwanda kujiendesha kibiashara kwa Kamati hiyo.

Aidha, Wajumbe wa Kamati hiyo walipata fursa ya kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali yaliyolenga kuboresha utendaji kazi wa KMTC ili kiweze kujiendesha wenyewe, kuongeza wigo wa utoaji huduma zake kuanzia kwenye viwanda hadi kwenye migodi ili kusaidia viwanda vingi vinavyohitaji vipuri na kuokoa fedha nyingi za kigeni zinazotumika kuagiza vipuri nje ya Nchi.

Naye, Waziri wa Viwanda na Biashara Dkt. Selemani Jafo akiwa ameambatana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara Dkt. Hashil Abdallah, ameihakikishia kamati hiyo kuwa wizara yake itayafanyia kazi maoni na mapendekezo yote.

Aliahidi kushirikiana na kamati hiyo katika kuhakikisha kiwanda hicho cha msingi kinachotengeneza vipuri kwa ajili ya viwanda vingine kinafanya kazi kwa tija na ufanisi katika kuendeleza sekta ya viwanda na biashara.

Aidha, ametoa wito kwa Watanzania hususani wamiliki wa Viwanda kupenda kununua na kitumia vipuri mbalimbali vya zinazotengenezwa na KMTC ili kukilinda na kuviwezesha kuendelea na uzalishaji, kuongeza ajira, Pato la Taifa na kuendeleza Viwanda na kukuza uchumi wa Taifa kwa ujumla.

Naye, Mkurugenzi Mwendeshaji wa Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) Dkt. Nicolaus Shombe akitoa elimu kwa wajumbe hao ameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuiwezesha NDC kutekeleza ipasavyo majukumu yake.



# Rais Dk. Samia mitano tena

NA MWANDISHI

**MAELFU ya wananchi wakionekana kuridhishwa na utendaji wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan wameendelea kusisitiza ni lazima wampe kura zote katika Uchaguzi Mkuu mwaka huu kwani wanataka akamilishe miaka yake mitano tena.**

Hayo yanaonekana kutoka pande zote za nchi, huku bado wananchi wakiendelea kuchanga fedha za kumchukulia fomu ya kugombea Dkt. Samia wakikiri kuridhishwa na utendaji wake kazi.

Wakati walimu, waendesha bodaboda, wajasiriamali, wanafunzi na watu wa kada mbalimbali wakiendelea kumchangia fedha ya kuchukulia fomu Dkt. Samia kuonesha kukunwa na utendaji wake, mwishoni mwa wiki watu wa Chato nao waliamua kufanya hivyo.

Wakazi hao wa Chato, Geita walijitokeza kumchangia Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kiasi cha Sh milioni 1.4 kwa ajili ya kuchukua fomu ya kugombea nafasi ya uraisi katika uchaguzi mkuu mwaka 2025.

Mchango huo umefanyika katika hafla maalum iliyoandaliwa na Kamati ya Amani ya Wilaya ya Chato inayoundwa na viongozi wa dini mbalimbali kwa ajili ya kuliombea taifa dhidi ya ugonjwa wa Marburg.

Ikumbukwe kuwa hivi karibuni serikali ya Tanzania ilithibitisha kuwepo kwa ugonjwa wa Murburg wilayani Biharamulo mkoani Kagera ambapo ni jirani na Chato.

"Kwa hiyo huko asijitokeze mwingine anataka kumchukulua mama fomu, wana Chato tumechanga pesa ya kutosha Mama Samia kuchukua fomu kwenye maombi ya kuiombea nchi wanachato tumeshachanga," alisema Mwenyekiti wa Kamati ya Amani ya wilaya, Sheikh Abdalah Aman Isimail.

Uchunguzi uliofanywa katika mikoa mbalimbali unaonesha uteuzi wa wagombea hao umekata kiu waliyokuwa nayo kutaka wasimame tena kuwania nafasi zao ili kuendeleza mambo makubwa ya maendeleo waliyoyafanya.

Dkt. Samia amejipambanua kwa mengi, kwani kwa sasa anawekewa mikakati maalum vijana kuhakikisha wanaendana na mabadiliko, ikiwa pia kuwaandaa na taaluma na ujuzi zinazoendana na mageuzi ya teknolojia mpya.

Haya yamebainishwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan mwishoni mwa wiki, ambapo pia alizitaka Wizara ya Fedha, Wizara ya Mipango na Uwekezaji, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais-TAMISEMI, kuwezesha na kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Sera na Mitaala mipya ya Elimu, ili ilete matokeo yaliyokusudiwa katika kuimarisha sekta ya elimu.

Katika hili la elimu, Dkt. Samia alisisitiza, ili kuendana na mabadiliko ni lazima kutumia TEHAMA kutoa elimu kwa urahisi na kuwandaa vijana wetu kuwa na taaluma na ujuzi wa taaluma zinazoenda na mageuzi ya TEHAMA bila kuathiri maadili ya vijana hao.

# Uchumi unavyopiganiwa Songea

NA ALBANO MIDELO, Songea

**SERIKALI kwa kushirikiana na wananchi wa halmashauri ya Madaba wilayani Songea mkoani Ruvuma wameanzisha shamba kubwa la miti lililopo Wino ambalo ni la tatu kwa ukubwa Tanzania.**

Mkuu wa Wilaya ya Songea, Kapenjama Ndile, amesema shamba hilo linaonesha jinsi ambavyo Songea haipo nyuma katika utunzaji wa mazingira, na shamba hilo linaweza kubadilisha na kuchochea uchumi wa na nchi.

Amesema shamba hilo ambalo linasimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS ) limekuwa likizalisha mbegu na miche mbalimbali na kusambaza kwa wananchi vijijini ili kuendelea kutunza mazingira na wawekezaji wakubwa wa kuchakata mazao ya misitu wako mbioni kujenga viwanda katika Halmashauri hiyo.

Kwa upande Meneja wa shamba hilo, Groly Kasmir, amesema shamba hilo lina ukubwa wa heka 39,714, kati ya hizo heka 2,259 zipo Wino, 29,000 zipo Ifinga na 9,000 zipo Mkongotema.

Ameeleza kuwa mpaka sasa miti waliyopanda ni misindano na mwaka huu wanatarajia kupanda miti aina ya mikaratusi kwa ajili ya nguzo kwa kuwa mazingira yanaonesha kuna uwezekano na miti hiyo kustawi.

# Mabadiliko tabia nchi ni muhimu kujua

NA MWANDISHI WETU

**WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma umeendelea na juhudi za kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kulinda misitu ili kuepuka athari za mabadiliko ya tabianchi.**

Meneja wa TFS Wilaya ya Songea, Mhifadhi Issa Mlela, amewataka wananchi kushirikiana na serikali kudhibiti ukataji miti holela, ambao unaweza kusababisha ukame na kuathiri kilimo cha chakula na biashara.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mlela amesema kuwa misitu ni rasilimali muhimu kwa kuhifadhi mazingira na vyanzo vya maji, hivyo uharibifu wake unasababisha madhara makubwa kwa jamii.

Ameeleza kuwa TFS inatumia vyombo vya habari na mikutano ya kijamii kutoa elimu juu ya athari za uharibifu wa misitu na umuhimu wa kuilinda.

# Utamaduni na fursa ya kukuza utalii

NA MWANDISHI MAALUM



**MAISHA siku zote yamekua ni kujifunza kutokana na wengine na kujifunza kutokana na vitu mbali mbali ambavyo vimetokea na vinavyotokea kila kona ya dunia.**

Ukweli ni kwamba katika kujifunza vitu mbali mbali hakuna anayeweza kupata vitu vyote kwa wakati mmoja na kujifunza na kufahamu kila kitu.

Maisha yamekuwa na maana nyingi sana kutokana na maeneo ambayo watu wanaishi, utamaduni na hata Imani. Dunia ina kila aina ya watu ambao wana aina yao ya maisha ambayo ni tofauti na maisha tunayoyaishi sisi au tulioyazoea kuyaona mara kwa mara.

Dunia bado ina mambo na vitu vizuri na vya kushangaza vinavyofanywa na watu mbali mbali kutokana na tamaduni, sehemu wanazoishi na mfumo wa maisha yao.

Tangu dunia iumbwe na watu waumbwe kumekuwa na mtawanyiko mkubwa sana ambao umesababisha watu kuwa na mifomo tofauti tofauti ya maisha, mifumo hiyo tofauti ndio imetufnya kuwa tofauti.

Kuna sehemu hapa duniani watu wanakula vitu ambavyo wewe huwezi kula, kuna sehemu hapa duniani watu wanafanya vitu ambavyo wewe huwezi kufanya wala hujawahi kufikiri kama kinaweza kufanyika. Kuna watu hapa duniani wanaishi maisha ambayo wengine hawawezi kuyaishi kabisa. Hivyo ndivyo binadamu alivyoumbwa na uwezo mkubwa wa kuishi vyovyote na wa kufanya vitu tofauti tofauti. Hapo bado sijaweka maswala ya imani, kuna watu wanaamini vitu ambavyo wengine hawawezi kuamini kabisa, wana Imani tofauti kabisa na wengine.

Tofauti hizi ndio zinafanya maisha kuwa na mvuto wa kipekee, sisi binadamu huwa tunapenda sana vitu vya kushangaza na kuvutia, hiyo ndio asili yetu, tunapenda kuona na kusikia vitu visivyo vya kawaida hasa kama vimefanywa na wanadamu wenzetu.

Kwa asili tunapenda miujiza na kuona vitu vikubwa vinavyofanyika hata nje ya upeo wa maisha yetu, binadamu tunapenda kushangazwa, tunapenda kuona vitu vipya vikitokea.

Hii ndio maana Mungu alituweka sehemu tofauti tofauti na tuishi maisha tofauti tofauti yasiyofanana na mtu mwingine.

Kama hiyo haitoshi, kwenye nchi yaani ndani ya nchi husika sio watu wote wanafanana na sio wote ni weupe na sio wote ni weusi.

Kwa mfano nchi ya Tanzania ina zaidi ya makabila 120, haya makabila yote yasingekuwepo kama hakuna utofauti kati yao, kuna utofauti mkubwa sana kwenye masuala mengi sana hasa ya utamaduni, mila na desturi, mfumo wa maisha na hata lugha zao za asili zinatofautiana, hata vyanzo vya kipato na njia za kujipatia chakula zinatofautiana.

Ndio maana sehemu nyingine ni wafugaji na sehemu nyingine ni wakulima, sehemu nyingine wanalima mahindi pekee sehemu nyingine wanalima mpunga, sehemu nyingine ni wavuvi, sehemu nyingine wanalima kahawa na sehemu nyingine hawalimi kabisa kahawa tena wanaweza wasijue chochote kuhusu kahawa labda kama wamesoma shuleni au sehemu nyingine.

Kwanini naandika haya yote, ni kwasababu nataka kuweka mambo kwenye msitari mmoja ya kuwa maisha yana maana mbali mbali kwa watu tofauti tofauti, usiyafikiri na kuyaamulia maisha kwa tafsiri yako mwenyewe kwenye eneo dogo unalojua la Kijiji au nchi yako.

Kumbuka kuna maisha ambayo hujayajua na hujayaishi hivyo fikra na mawazo yako yasihitimishe kuwa maisha yana rangi ya moja pekee.

Maisha yana rangi nyingi sana ambazo umeziona wewe kuna wengine wameziona nyingi zaidi ya hizo rangi, na kuna wengine hawajaona rangi yoyote, hivyo kwa mantiki hii ndipo linapokuja suala la elimu kuwa haina mwisho na kujifunza hakuna mwisho. Ni mjinga pekee ndiye anaye weza kufkiri na kujiaminisha kuwa ameshajifunza na kufahamu kila kitu kwenye maisha.

Aidha kwa kutambua jambo hili, nchi mbali mbali zimekuwa makini sana kuhakikisha zinatumia njia mbali mbali kwa ajili ya kuhifadhi na kutunza utamaduni na vitu mbali mbali vinavyoonyesha utamaduni na maisha ya watu wa kale walioishi aina fulani ya maisha tofauti na sisi wa leo. Utamaduni una nafasi yake kubwa sana kwenye nchi yoyote, utamaduni umekuwa ndio kitambulisho kikubwa kwa nchi na mataifa mbali mbali hapa duniani.

Na kwasababu watu wapo tofauti hivyo na utamaduni ni tofauti na hapa ndipo maisha yanakuwa na mvuto wa kipekee. Kila nchi ina utamaduni ambao inakubali na inautunza kwa gharama zote.

**Itaendelea kesho**



# Mbwa Mwitu ni Mwindaji Katili?

**MBWA mwitu wa Afrika (African wild dog), ni mnyama jamii ya Kanivora (Carnivorres) kwa maana ya wanyama wanaokula nyama. Wanyama hawa wana mdomo mrefu na kucha zisizoweza**

**kujificha (unsheathed claws**

Katika kundi hili la mbwa mwitu kuna wanyama pia kama mbweha (fox) mbweha masikio (bat eared fox). Vile vile wanyama hawa wana meno marefu ambayo husaidia wakati wa uwindaji na wana vidole vinne katika miguu ya mbele.

Mbwa mwitu ni mnyama ambae asili yake ni porini na anapatikana katika bara la Africa tu na ni tofauti na watu wanavvodhani kwamba wana asili moja na mbwa wa majumbani bali wana utofauti mkubwa sana kitabia na namna wanvyoishi, kwani watu wengi wanadhani mbwa mwitu wana asili sawa na mbwa wa majumbani na badaye kwenda kuishi mwituni (tabia inaitwa feral)

Mbwa mwitu wa Afrika amekuwa akidhaniwa kuwa ni mwindaji katili sana, je ni kwanini? Kabla hatujajua zaidi kuhusu tabia hii, basi hebu tujifunze kidogo kuhusu tabia za mbwa mwitu

Maisha na tabia za mbwa mwitu wa Africa

Mbwa mwitu wa Afrika ni hodari katika uwindaji na ustadi mkubwa kwani wanauwezo mkubwa wa kunusa, kuona hasa nyakati za usiku (japo hawawindi sana usiku), pia uwezo wa kusikia sauti mbali mbali. Mbwa mwitu wote huwinda sawa, maana wanaumoja wa hali ya juu sana.

Mbwa mwitu wa Africa wanaishi katika kundi ambalo baba na mama huongoza familia yao. Mbwa mwitu hawana ndoa za mitala yaani mahusiano yao yanahusiana na baba na mama mmoja tu. Watoto wanaozaliwa, jike anaruhusiwa kuhama na kwenda kutafuta dume sehemu nyingine, huku dume anabaki kuendeleza ukoo au kundi.

Mbwa mwitu wa Afrika, hawana mipaka ya kuishi kwani hawana makazi ya kudumu, bali wanatulia sehemu moja pale tu mbwa jike akizaa ili kulinda watoto wanaishi katika bonde au eneo fulani mpaka watoto wakue ndipo wataanza kuhama hama. Hawalindi mipaka kama ilivo kwa mbweha miraba na mbweha masikio

Mbwa mwitu wa Africa dume anahusika katika kulea watoto kwa kwenda kutafuta chakula ili jike aweze kunyonyesha watoto. Baada ya hapo wana uwezo wa kucheua chakula walichokihifadhi tumboni ili kuwalisha wengine mfano watoto na wale wasiojiweza kuwinda kwa nyakati fulani.

Vile vile wana uwezo wa kufukia chakula chini na kutumia chakula kwa muda mwingine na alama kama harufu ya mkojo hutumika kutambua alipofukia chakula.

.Pia mbwa mwitu kila mmoja ana mpangilio wa kipekee wa rangi na madoa ya ngozi zao hivyo kutambuliwa kirahisi kundini. Mbwa mwitu wa africa wanapojamiiana dume na jike wanageuziana mikia hii kwa sababu dume huchelewa kutoa mbegu na hivyo kumfanya jike kubana uume wa dume mpaka akisha mwaga mbegu. Hivyo wakigeuziana mikia husaidia kujilinda na kumaliza tendo salama kwani hujamiiana mara moja tu.

Wanapiga kura kwa chafya ili kutoa maamuzi ya kulala, kupumzika, kuwinda, au kupambana na adui. Hivyo kwenye kundi kiongozi ndiye atakae angalia idadi ya mbwa wengine waliopiga chafya ili kutoa maamuzi.

Mfano wakipiga chafya kwa wingi na kwa nguvu wakiona windo hii hutoa ishara ya kwenda kuwinda, hivyo kiongozi huamrisha kundi ili kuwinda mara moja na wote huvamia windo. (Jaribu kumchunguza hata mbwa wa nyumbani kukiwa na hatari huwa anafanya kama kupiga chafya, je hii ni kwaida ya mbwa au ni lazima)

Fahamu kuwa mbwaa mwitu ni muwindaji hodari na ana ustadi mkubwa sana, kama ilivyo kwa wanyama jamii ya paka yaani samba (Lion), simbamangu (caracal), duma) Cheetah) , chui (Leopard), mondo (Serval) nk.

Watu wengi tunafikiria kuwa mbwa mwitu ni muwindaji katili, kwa sababu huwa wanasabisha kifo chenye maumivu endelevu kwa windo lao. Kwani wanauwezo wa kumla mnyama hata kama bado mzima, kwa kumtafuna na kung'ata sehemu nyeti za windo kama vile tumbo, korodani na miguu ili kufanya windo asiweze kutembea au kukimbia. Hali hiihusababisha windo kutoka damu nyingi na kupoteza nguvu hadi kufa.

Sababu zinazofanya Mbwa mwitu awinde kwa namna hii;

Umbo dogo la walilonalo wanyama hawa hutumika kumparua kidogo kidogo kwa kumzingira mpaka mnyama (windo) kudondoka chini, Mfano swala, pundamilia na nyumbu na kisha kuanza kumla mnyama akiwa bado mzima, tabia hii ipo hata kwa fisi.



# Nunga; Swala aliye hatarini zaidi kutoweka



NA MWANDISHI WETU

**NI siku nyingine tena wasomaji na wadau wa makala hizi za wanyuamapori bila kuwasahau wahifadhi na mamlaka zote za uhifadhi wa wanyamapori hapa nchini.**

Tunakutana tena katika darasa letu huru la wanyamapori na kujuzana mengi yenye manufaa kuhusu wanyamapori na faida ya uwepo wa wanyama hawa hapa nchuni hasa kwenye pato la taifa.

Bila kusahau changamoto mbali mbali zinazo wakumba wanyama hawa hasa kwenye maweneo yao asilia na hapa nikimaanisha katika hifadhi za taifa na mapori ya akiba ya uhifadhi wa wanyamapori.

Kama kawaida nakuletea makala nyingine tena ambayo kwa hakika utafurahia uchambuzi wa mnyama kwenye makala yetu ya leo kwani kuna sifa kubwa sana na kujivunia sana kwa uwepo wa mnayama huyu hapa nchini. Tuna kila sababu ya kupenda vilivyo vyetu na kuvitunza tena kwa umakini na moyo wa kujitolea kwa ari na nguvu zaidi.

Tanzania ni moja kati ya nchi pekee duniani inayo jivunia uwepo wa idadi kubwa na jamii nyingi za wanyamapori. Nasi kama watanzania hatunabudi kutembea vifua mbele kwa kujivunia kuwa watanzania na kuwa na rasilimali nyingi hapa nchini hasa kwa upande wa wanyamapori. Moja kati ya sababu zinazo ifanya Tanzania kuwa ya kipekee hususani kwenye suala la uwepo wa jamii nyingi za wanyamapori ni mazingira rafiki kwa wanyamapori lakini pia mipango mikakati ya usimamizi na ulinzi wa rasilimali hii.

Katika makala haya nimepanga kukujuza mambo machache na yenye kuvutia kuhusu mnyama jamii ya swala ambae mnyama huyu anapatikana nchi 2 tu duniani kote na katika nchi hizo mbili ni baadhi maeneo matatu tu ambayo mnyama huyu anapatikana. Tanzania ni moja kati ya nchi hizo mbili zinazo jivunia uwepo wa swala huyo.

Mnyama huyo jamii ya swala hujulikana kama NUNGA au PAA NUNGA (Aders' duiker). Jina lake la kisayansi anajulikana kama Cephalophus adersi. Swala huyu hapa nchini anapatikana Zanzibar tu.

Japo kuna majina mengi kuhusu mnyama huyu kama Mwalimu, Kungu marara, Harake na Guno (majina matatu ya mwisho ni kwa nchini Kenya), ila jina maarufu hususani kwa hapa nchini Tanzania swala huyu hujulikana kama Nunga.

Mnyama nunga pia ni miongoni mwa wanyama katika kundi la wanyama jamii ya swala ambae kwa haraka haraka kwa watu ambao sio wataalamu wa wanyamapori wanaweza kumchanganya mnyama huyu na digi digi kwani wanafanana sana na utofautii sana zaidi upo kwenye ukubwa wa miili yao.

Kwa wataalamu wa wanyamapori basi ni rahisi sana kuweza kuwatofautisha nunga na digi digi kwani wana utofauti mkubwa sana. Nunga ni miongoni kati ya swala wazuri na wenye kuvutia sana katika kundi la wanyama jamii ya swala. Katika swala watatu wazuri basi huwezi kumuacha nunga.

**SIFA NA TABIA ZA NUNGA**

Miili yao imezungukwa na manyoa malaini sana mfano wa Hariri huku ngozi yao ikiwa nyembamba na laini sana.

Sehemu ya mbele usoni wana manyoa mengi yenye rangi ya wekundu inayo ng'aa.

Sehemu ya juu mkiani, kwenye sehemu ya juu miguu ya nyuma na mgongoni wana rangi ya kahawia ambayo inataka kuelekea kwenye wekundu huku kadri unavoelekea maeneo ya shingoni wana rangi ya kijivu.

Sehemu ya chini tumboni wana rangi nyeupe inayong'aa na mstari ambao unaunganisha rangi nyeupe na nyekundu mpaka sehemu ya paja na nyuma. Mstari huu ni alama ya kipekee inayo patikana kwa nunga hawa tu na si jamii nyingine.

Wana miguu yenye rangi ya wekundu ambayo karibu na kwato rangi hubadilika na kuwa nyeusi. Miguu yao ina alama ya vidoti vyeupe hasa miguu ya mbele.

Wana kishungi chenye rangi ya wekundu sehemu ya kichwa. Wote madume na majike wana pembe ndogo zenye urefu wa sentimita 3-6 na masikio yenye urefu wa sentimita 7-8.3.

Sehemu ya pua na mdomo vimechongoka huku ncha ya pua ikiwa ni bapa. Sehemu ya shingoni pia wana alama ya manyoa ambayo yametengenezeka mfano wa duara.

Nunga ni miongoni mwa wanyama jamii ya swala wenye aibu sana na wana uwezo mkubwa sana wa kusikia na kujificha hasa wanapohisi kuna kitu tofauti kwenye mazingira yao.



# Unapokumbana na bidhaa bandia

NA MWANDISHI MAALUM



**MARA nyingi tunanunua vitu na bidhaa mbalimbali bila kuzifahamu au kuzichunguza vyema Hili limepelekea watu wengi kununua bidhaa zisizofaa kwao au zenye madhara kwenye afya zao.**

Kutokana na ukosefu wa elimu pamoja na kuishi kwa mazoea, watu wengi hawajui wala hawachunguzi vyema bidhaa wanazozinunua ili kuhakikisha ubora wake.

Madhara ya kutumia bidhaa bandia ni mengi na baadhi ni matatizo ya kiafya kama vile saratani na ulemavu, upotevu wa fedha, ajali (milipuko au shoti ya umeme) na kuathiri uchumi.

Ni wazi kuwa yapo madhara mengi yatokanayo na matumizi ya bidhaa feki, hivyo ni vyema ukafahamu njia za kubaini bidhaa hizi.

**1. Matangazo Yasiyo Ya Kawaida**

Wahenga walisema 'Chema chajiuza kibaya chajitembeza', ni vyema ukawa makini na bidhaa zenye punguzo kubwa la bei kuliko kawaida, kwani mara nyingi bei hupungua sana kutokana na ubora duni.

Pia ni vyema ukaepuka kuvutiwa na maneno ya kibiashara kama vile 'Oringinal', 'Collection', 'King Size', 'Royal', 'Genuine', 'Real', 'Authentic', 'Mpya' au 'Kali'.

Kumbuka simaanishi usinunue bidhaa yenye punguzo au maneno haya bali yasiwe ndiyo yanatawala au kutumiwa kama mbinu ya mauzo.

**2. Fahamu Bidhaa Yako**

Ni vyema ukaichunguza na kuifahamu bidhaa ambayo unainunua au kuitumia mara kwa mara.

Hili litakuwezesha kubaini bidhaa ambayo ni bandia kwa urahisi zaidi. Chunguza na bainisha vitu vya msingi ambavyo ni lazima viwepo kwenye bidhaa husika.

Hivyo kabla ya kununua bidhaa hakikisha inafanana na ile uliyoizoea, kama hujawahi kuinunua unaweza kumwomba mtu anayeifahamu vyema akusaidie kuikagua.

**3. Kakagua Vifungashio**

Kubaini bidhaa bandia kunahitaji utulivu, chukua muda kukagua vifungashio vya bidhaa husika kwa makini.

Hili litakuwezesha kubaini kukosekana kwa taarifa muhimu kama vile jina la mtengenezaji, mahali pa utengenezaji, tarehe ya kuzalishwa na ya mwisho wa matumizi pamoja na taarifa nyingine muhimu.

Bidhaa iliyokosa taarifa muhimu inaweza kuwa bandia au yenye ubora duni.

**4. Kila Kilichotakiwa Kuwepo Kipo**

Mara nyingi unaweza kununua kifaa au bidhaa yenye kitu zaidi ya kimoja Kwa mfano, ikiwa unanunua simu au kamera hakikisha kama huwa inauzwa pamoja na vifaa kama vile betri, chaja, memory card na waya wa USB vipo vyote tena kwenye hali nzuri.

Mara nyingi bidhaa bandia hukosa baadhi ya vifaa muhimu ambavyo kwa kawaida huwepo kwenye vifaa au bidhaa halisi.

**5. Jitahidi Kuuliza Kuhusu Warranty**

Warranty ni mkataba maalumu baina ya mnunuzi na mtengenezaji wa bidhaa husika.

Warranty hukuwezesha kutengenezewa au kubadilishiwa bidhaa husika ikiwa itapata matatizo ndani ya muda fulani.

Bidhaa bandia kamwe huwa hazitoi Warranty na zikitoa basi ni bandia pia. Hivyo ni vyema ukatazama kama bidhaa husika (Hasa vifaa vya kielektroniki) zina Warranty ya uhakika.

**6. Tembelea Tovuti Ya Mzalishaji**

Hivi sasa karibu kila kampuni imejitahidi kufungua tovuti kwa ajili ya kuwafikia wateja wake kwa urahisi zaidi.

Pia kampuni nyingi zimekuwa zikijitahidi kuwawezesha wateja wake kubaini bidhaa feki.

Wakati mwingine, baadhi ya bidhaa huwekwa namba ambazo unaweza kuziingiza kwenye tovuti yao na kuona kama bidhaa ni bandia au laa.

Hivyo, unaweza pia kutumia njia hii ili kubaini na kuepuka bidhaa bandia.

**7. Wakala Aliyeidhinishwa**

Ili kurahisisha na kuhakikisha ubora wa huduma, kampuni nyingi zimekuwa zikisajili mawakala kwenye maeneo mbalimbali.

# M23 wanapotuliza kwa kuitaka Goma

**VITA Goma ndani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo inazidi kushika kasi, huku Tanzania na yenyewe ikijikuta ikipoteza askari wake wawili mujibu wa Taarifa iliyotolewa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).**

Wanajeshi hao walifariki kutokana na mfululizo wa mashambulizi yaliyofanywa na wapiganaji wa M23 katika maeneo ya Sake na Goma.

Taarifa hiyo imeongezea kuwa wanajeshi wengine wanne waliojeruhiwa wakati wa shambulio hilo wanapokea matibabu mjini Goma.

Taarifa hiyo iliyotiwa saini na Kaimu Mkurugenzi wa Habari na Uhusiano wa JWTZ, Kanali Gaudentius Gervas Ilonda imesemna kwamba taratibu za kusafirisha miili ya marehemu pamoja na majeruhi zinaendelea kupitia sekretariati ya SADC.

Ila mpaka sasa unajiuliza, kwa nini Mji wa Goma nchini DRC ni muhimu na kwa nini waasi wa M23 wanautaka?

Mji wa Goma ulio mashariki mwa DRC umekuwa tena kitovu cha mzozo wa kikanda uliodumu kwa miongo kadhaa. Mapigano kati ya kundi lenye silaha linalojulikana kwa jina la M23 na jeshi la Congo yamezidi katika eneo hilo, na kuwafukuza zaidi ya watu 400,000 kutoka makwao tangu mwanzoni mwa mwaka huu.

Lakini kwanini Goma?

Kundi la M23 ni kundi lenye silaha ambalo lilijitenga na jeshi la Kongo miaka kumi iliyopita kwa madai ya kuwalinda Watutsi ambao kwa muda mrefu walikuwa wakilalamikia mateso na ubaguzi.

Wataalamu wa Umoja wa Mataifa wanasema kuwa kundi hilo linaungwa mkono na nchi jirani ya Rwanda, ambayo pia inaongozwa na Watutsi, jambo ambalo Serikali ya Rwanda imekuwa ikikanusha mara kwa mara.

Rwanda imesema hapo awali kwamba mamlaka nchini DR Congo inashirikiana na baadhi ya waliohusika na mauaji ya kimbari ya mwaka 1994 dhidi ya Watutsi na Wahutu wenye msimamo wa wastani.

Mwaka 2012, waasi waliikalia Goma kwa siku 10 kabla ya kuiacha kufuatia shinikizo la kimataifa.

Baada ya hayo, kundi la M23 lilipata pigo baada ya kushindwa vibaya na jeshi la Congo likisaidiwa na jeshi la kimataifa ambalo lilishuhudia kufurushwa kwao kutoka nchini humo. Wapiganaji wa M23 kisha walikubali kushirikishwa tena katika jeshi kwa ahadi kwamba Watutsi watalindwa.

Lakini, mwaka 2021, kundi hilo lilichukua tena silaha, likisema ahadi zilikuwa hazijatimizwa.

M23 tangu wakati huo wamechukua udhibiti wa maeneo mengi zaidi katika eneo la mashariki kuliko hapo awali. Wataalamu wa Umoja wa Mataifa wanasema Rwanda ina hadi wanajeshi 4,000 wanaofanya kazi pamoja na M23 mashariki mwa Kongo DR.

Eneo la Goma

Likiwa kwenye ufuo wa kaskazini mwa Ziwa Kivu kwenye mpaka wa Rwanda, Goma daima imekuwa kitovu muhimu cha kisiasa na kibiashara.

Mji huo una watu zaidi ya milioni moja na kuufanya kuwa moja ya miji yenye watu wengi zaidi Kongo. Kutokana na udongo wake wa volkeno, wenye rutuba kihistoria mji huo umekuwa kituo cha biashara chenye shughuli nyingi na nchi jirani ya Rwanda.

Goma ni mojawapo ya miji mikuu ya uchimbaji madini inayosambaza madini yanayohitajika sana kimataifa kama vile dhahabu, bati, kobalti na koltani na ina barabara muhimu za kimkakati za usafiri wa barabarani na angani. Pia ina kambi kubwa ya walinda amani wa Umoja wa Mataifa suala ambalo limevutia biashara nyingi, mashirika ya kimataifa na balozi.

Utajiri wa Goma

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo inakadiriwa kumiliki asilimia 70 ya madini ya cobalt duniani, madini muhimu katika kuwezesha betri za lithiamu-ion katika simu za mkononi, magari ya umeme na aina nyingi za sigara za kielektroniki.

Huku ulimwengu unapojitolea kupunguza utoaji wa gesi chafuzi kwa kuhama kutoka kwa nishati ya kisukuku, kuna ongezeko la mahitaji ya vyanzo safi vya nishati.

Tishio la vita vipya vya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo linaweza kuvuruga ugavi wa kimataifa, kupanda kwa bei na kusababisha uhaba katika tasnia ya teknolojia na nishati safi.

Goma inapotekwa

Rais wa DRC Felix Tshisekedi mwaka 2023 alisema kuwa "Goma haitatekwa kamwe". Ahadi zake za kuhakikisha kuwa mji huo hauna waasi zilikuwa juu kwenye orodha yake ya ahadi kwa watu wa nchi hiyo, ikimaanisha kutekwa kwa Goma kungemuathiri kisiasa kiongozi huyo aliyechaguliwa tena.

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo imekata uhusiano wote na nchi jirani ya Rwanda, jambo ambalo limesababisha onyo kutoka kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres kwamba mzozo wa sasa unaweza kuhatarisha kuongezeka kwa vita vya kikanda.

Kuongezeka kwa mzozo kunaweza pia kusababisha uhaba wa rasilimali za kibinadamu ambazo tayari zimepungua kutokana na machafuko mengine.

Wakati M23 inasonga mbele katika eneo la mashariki, maelfu katika vijiji vidogo wanayahama makazi yao na kuelekea katika hospitali za karibu huko Goma, jambo ambalo linawalemea.

Shirika la kutetea haki za binadamu la Human Rights Watch limeonya juu ya kuongezeka kwa hatari kwa raia huku jeshi likipambana na waasi wa M23. Kundi la misaada ya kibinadamu linashutumu pande zote mbili kwa kutekeleza unyanyasaji mkubwa dhidi ya raia.






# Usilale, inuka upambane kwa biashara hizia

NA MWANDISHI WETU

**UNAWEZA kulia njaa, lakini kuna biashara ndogondogo zenye faida kubwa na ambazo zinalipa na pia zinazohitaji mtaji kidogo ili kuanzisha pamoja na kuiendesha.**

**1. Juisi ya Matunda**

Ukiwa na Sh 10,000 mkononi unaweza kuanzisha biashara hii na inaweza kukupa hadi lita kumi za juisi ambapo lita moja ni sawa na glasi tano au nne. hivyo kwenye lita kumi utapata grasi 40 ambazo zitakupa Sh 20,000 na ukitoa gharama nyingine kama sukari utapata faida ya Sh 5,000.

**2. Matunda**

Siku hizi watu wengi hasa maofisini wanapenda kula matunda muhimu ni Kuzingatia usafi wako na bidhaa yako, hapa unaweza kutumia kama Sh 15,000.

Unanunua matunda mchanganyiko, nunua vifungashio vile vya kuwekea matunda yako ambapo yakiuzika na biashara ikaenda vyema unaondoka na faida nusu kwa nusu

**3. Mkaa**

Kwenye biashara ya gunia la Sh 30,000 unaweza kutoa mafungu 45 ya mkaa sawa na Sh 45,000 faida Sh 15,000.

**4. Genge linalotembea**

Biashara ya genge linalotembea unaweza kutumia simu yako kutangaza unauza vitu vya gengeni kama nyanya, vitunguu karoti, na vitu vingine ya jikoni, ukipata oda unaenda soko la wakulima, unanunua vitu vya jumla vya kutosha faida hapa ni nusu kwa nusu, pia unaweza tembezea majirani zako kutegemeanana sehemu unayoishi

**5. Vitafunwa**

Biashara ya vitafunwa kama crips, sambusa, chapati, maandazi, mihogo ya kukaanga, vitumbua karanga za mayai, ubuyu, korosho, visheti na bites zingine unaweza kufanya biashara ya kusambaza vitafunwa maofisini kwa 'package' au ukauzia nyumbani moja ya vitafunwa hivyo

**6. Vinywaji baridi vituo vya mabasi**

Unaweza ukauza hata kwenye ndoo kama huna deli nunua mabarafu nunua vinywaji tafuta kijana au wewe mwenyewe uza biashara yako kwenye stend za daladala inalipa saaana

**7. Uji wa ulezi, uji wa mchele**

Biashara ya uji wa mchele pamoja na uji wa ulezi ni biashara nzuri sana unaweza kuanza kwa kukodi toroli jaza chupa zako uji aina hizo tembeza kwenye magereji na sehemu za bodaboda.





# Zifahamu Hifadhi za Taifa zilizopo Kusini-2

NA MWANDISHI MAALUM

**ZIPO hifadhi nyingi Tanzania, lakini ngoja tuzitazame zile zilizopo Kanda ya Kusini na baada ya hapo tuzijue hatua ambazo zikifuatwa zitasaidia kuinua utalii ukanda huo.**



Tanzania ni miongoni mwa nchi chache barani Afrika zinazotembelewa na watalii wengi sana kutoka pande zote za dunia.

Wageni wengi ambao wanaingia huja kufanya utalii wa wanyamapori hasa ambao wapo kwenye Hifadhi za Taifa (TANAPA) na mara chache hufanya kwenye mapori ya akiba kutokana na miundo mbinu kutokuwa imeimarishwa mfano mahoteli, barabara na ofisi pia ambazo nyingi zipo nje na mbali ya maeneo hayo.

Ukanda huu wa kusini hifadhi zake zinapatikana kusini mwa Tanzania ambazo zipo nne, Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Mikumi, Milima ya Udzungwa na hifadhi ya Mwalimu Nyerere (ambayo hapo zamani ilijulikana kama pori la akiba la Selous).

Ukanda huu una vivutio vingi vya utalii ukiachana na wanyamapori waliopo kwenye hifadhi za taifa pia kuna wanyamapori waliopo kwenye mapori ya akiba mfano Mpanga-Kipengele, misitu ya asili na yenye historia za makabila kama msitu wa Nyumba nitu mkoani Njombe, vivutio vya kihistoria kama bonde la Isimila, Kalenga kwenye fuvu la Chifu Mkwawa, majengo ya wakoloni ambayo wametawanyika sana mjini Iringa.

Pia kuna baadhi ya sehemu za Mkoa wa Njombe na Mbeya, daraja kimaajabu daraja la Mungu lililopo mkoa wa Mbeya, maji moto, pia Ziwa Nyasa ambalo hutumika kama mpaka wa Tanzania na Malawi.

Kanda hii imekuwa ikipokea watalii wachache sana ukilinganisha na hifadhi za taifa zinazopatikana Ukanda wa Kaskazini. Uchache huu wa watalii umesababishwa na umbali ambao upo wa kutoka hifadhi moja kwenda nyingine kwa hizi za Ukanda wa Kusini pia umbali ambao upo kutoka kwenye jiji kubwa la katikati ambalo ni Dar es Salaam mpaka kuzifikia hifadhi hizi pana urefu mkubwa.

Miundo mbinu bado ni duni mfano kuifikia hifadhi ya taifa ya Ruaha kutoka Iringa mjini ni mwendo wa masaa mawili kwenye baranbara ya vumbi, hivyo inakuwa ngumu sana kufikiwa na watalii hasa wasio na uwezo wa kutumia ndege kutoka uwanja mkubwa wa ndege wa Dar es Salaam.

Bado ukanda huu huu hauna muamko wa shughuli za kitalii hivyo kumechangia hata wawekezaji kusita kujenga na kufungua mahoteli na majengo mengine ya kitalii.

Pia, hifadhi nyingi za ukanda huu zimeanzishwa baada ya uhuru hivyo hazikufahamika sana kwa kipindi kile cha wakoloni ukilinganisha na za ukanda wa Kaskazini ambazo zilianzishwa kabla ya uhuru mfano Serengeti iliyoanzishwa 1959 hivyo wakoloni waliweza kuzibeba mioyoni mwao na kwenda kusimulia uzuri wa hifadhi hizo kwa ndugu zao waliporudi makwao.

Hivyo basi, kwa nia moja ya dhati na mapenzi makubwa niliyonayo kwa ukanda huu wa kusini wenye vivutio vingi vya kitalii na ambao bado mazingira yake mengi hayajabadilishwa na binadamu.

Wizara husika inayosimamia mali asilia za taifa letu, TANAPA taasisi inayosimamia hifadhi hizi, makampuni yanayo shughulika na utalii yanayokaribisha na kuunganisha hifadhi zetu na watalii na wadau mbali mbali wa sekta ya utalii kwa ujumla pasipo kusahau jamii zinazoishi jirani na hifadhi za taifa za ukanda wa kusini na kwa hifadhi zote kwa ujumla.

# Tabia 10 za Tembo zinazofanana na binadamu-2

NA MWANDISHI WETU

**BINADAMU ni kiumbe mwenye sifa za kipekee ukilinganisha na viumbe wengine. Kibaiologia binadamu yaani spishi ya Homo sapiensi imekaribiana sana na wanyama jamii ya maswoke kwa takribani 99% ya vinasaba vyao vinafanana.**



Utafiti wa muda mrefu juu ya mnyama aina tembo umebaini baadhi ya tabia mabazo wanyama hawa wanzo zinafanana na zile ambazo binadamu anazifanya katika masiha yake ya kila siku. Kuna aina mbili za Tembo, ambazo ni Loxodonta Africana na Elephas Maximus. Makala haya itazungumzia juu ya tabia hizo za tembo ambazo zinafanana na zile za binadamu.

**Endelea…**

Mapenzi ya mama na mwana

Kama ilivyo kwa binadamu mama na mwana huonyesha upendo usio kifani. Mama hujitoa kumyonyesha kwa muda mrefu, kumlinda na kuhakikisha usalama wa mtoto hata kwa kujitoa maisha yake.

Vivo hivo tembo huwa na mapenzi makubwa kwa mwana, humyonyesha kwa takribani miaka mitano na muda wote huo mama hujitoa kwa ajili ya kumtunza na kumlinda mtoto dhidi ya maadui.

Ingawa usalama wa mtoto tembo huwa ni jukumu la tembo jike wote katika familia, ila mama huonyesha kuguswa sana na mtoto wake mfano tembo wanapovuka barabara, mama husimama barabarani na kuhakikisha mtoto wake amevuka ndipo naye avuke.

Kutokana na upendo wa mama na mtoto tembo mwenye mtoto huchukua tadhari sana na huwa tayari kupambana na kitu chochote kinachoweza kumkaribia au kumdhuru, hivyo haina budi kuchukua tahadhari kubwa unapomwona mwana tembo, usimkaribie ama kumchezea.

Kushirikiana dhidi ya maadui zao

Kama ilivyo kwa binadamu kusaidiana na hata kuwapa faraja wale wenye matatizo, tembo pia huweza kuwatambua wenzao wasipokuwa na furaha na kuwapa ulinzi pamoja na faraja.

Tembo huonesha tabia nyingi za upendo na kujali kama vile kutoa uchafu au kitu chochote kilichojishikiza kwenye wimili wa tembo menzao. Tembo wana hisia, kama furaha, huzuni na masononeko, na huweza kutambu hisia za tembo wenzao hivyo kushiriki hisia kwa kusaidiana.

Uwezo wa kutambua sura zao

Tembo ni miongoni mwa Wanyama wenye uwezo mkubwa wa kutambua uso wake. Hii imethibitishwa na jaribio liliofanywa kwa kuchora alama kwenye uso wa tembo na baadaye kumuwekea kioo.

Tembo alipojitazama kwenye kioo aliweza kugundua alama hiyo usoni mwake na kuanza kuifuta kwa kutumia mkonge wake, hii inathibitisha kuwa tembo anaujua uso wake. Pia tembo hutunza kumbukumbu za maadui wake aliyowahi kukutana nao. Watafiti wameeleza kwamba tembo huweza kuwatambua majangili ambao waliwawinda au waliowauwa wenzao hata kwa miaka mingi iliyopita.

Tembo huwa na desturi ya kutembeleana na kuwajulia hali wanafamilia ambao wametengana. Tabia hii imeonekana kwa tembo dume wanapoondoka kwenye familia huwa na tamaduni ya kuzitembelea familia zao za awali ili kuwasalimia.

Pia pale familia ya tembo inapotengana au kugawanyika kutokana na sababu mbalimbali mfano familia kubwa, migogoro na uhaba wa chakula tembo huendelea kudumisha undugu kwa kukutana mara kwa mara

Huwa na muda wa kustarehe

Binadamu huwa na desturi ya kutenga muda wa kustarehe kwa kufanya mambo mbalimbali vivo hivo kwa wanyama hawa hutenga muda pia wa kucheza na kufarahi. Mara nyingi Kuchezea matope, hukukaa na marafiki na kuogelea; kam sehemu ya wao kucheza.

Pamoja na kwamba tembo ameonyesha tabia hizi kumi ambazo zinafanana na baadhi ya tabia za binadamu bado binadamu ndiye adui namba moja wa tembo.

Ikumbukwe kwamba ni nadra sana porini kuona tembo anawindwa na wanyama wanaokula nyama kama vile samba, fisi,chui, mbwa mwitu na duma. Binadamu pekee ndio amekuwa chanzo kikuu ya kukatisha uhai wa wanyama hawa.

Ujangili utokanao na tamaa ya pesa na mali zimekuwa tishio kubwa kwa mnyama huyu. Vile vile migogoro kati ya binadamu na tembo nayo imefanya maisha ya wanyama hawa kuwa hatarini hususani pale wanapowaua kwa ajili ya kulipa kisasi pale tembo anapoharibu mazao.

Hatuna budi kupambambana kwa pamoja kupunguza mauaji ya Tembo na kupunguza migogoro kati ya binadamu na tembo ili kuwalinda tembo wetu.



# Urithi wa Dunia unapotakina nchini-2

NA MWANDISHI MAALUM

**KARIBU tena tujifunze maeneo yaliyopo Tanzania yenye urithi mkubwa kidunia yaliyobeba umuhimu katika historia na mali asilia.**



Kwanza fahamu, urithi wa ulimwengu ni kitu au sehemu fulani iliyokidhi vigezo stahiki vilivyowekwa kwa makubaliano ya wawakilishi wa mataifa mbalimbi sehemu hiyo itwe inaurithi wa dunia.

Tanzania ni miongoni mwa nchi 167 duniani zenye maeneo yenye umuhimu wa urithi wa kitamaduni au Urithi wa asili kama ilivyobainishwa na shirika la umoja wa mataifa la elimu, sayansi na utamaduni (UNESCO) chini ya sheria zake zilizoanzishwa mwaka 1972.

Maeneo yenye sifa za Urithi wa dunia, yalianzishwa kwa lengo la kuhakikisha Kuna ulinzi tosha katika tamaduni na maliasili zote zilizopo katika hatari ya kupotea na pia kuhakikisha kuna maendeleo endelevu yatokanayo na utalii wa vitu hivyo.

Tanzania iliipitia sheria hiyo na kuipitisha mnamo mwaka 1977 na kufanya maeneo yakemengi ya kihistotia kuwa na sifa na kuongeza idadi ya maeneo yenye urithi wa dunia. Mpaka Sasa Tanzania ina maeneo hayo Saba japokuwa mawili kati ya hayo yanapeperusha bendera ya kuwa hatarini kutoweka, kuharibika na kuhitaji ulinzi wa ziada. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

**5. Mlima Kilimanjaro**

Eneo hili la hifadhi ya taifa ya mlima Kilimanjaro liliongezwa kwenye orodha ya maeneo yenye urithi wa dunia mnamo mwaka 1987 mkoani Kilimanjaro kwa lengo la kuhifadhi na kutunza Mlima Kilimanjaro ambao ni mrefu zaidi Afrika wenye asili ya volkano.

Mlima huu wenye umaarufu wa kuwa na barafu inayooneka nyeupe kwa mbali katika vipindi vyote vya mwaka. Pia chini/ kitako Cha mlima kuna jamii za wanyama wakubwa tofauti tofauti ambao baadhi wapo hatarini kutoweka kama tembo.

**6. Mji Mkongwe**

Eneo hili lilitambulika kama eneo lenye Urithi wa dunia kwa upande wa historia mnamo mwaka 2000 likiwa visiwani Mashariki ya Tanzania bara. Eneo hili linabeba historia ya mwingiliano mkubwa wa tamaduni tofauti tofauti ambazo zimepelekea ukuaji wa mji huo kwa karne nyingi.

Hata hivyo mji mkongwe bado una masalia ya watu wenye asili ya Kiarabu, Kiajemu, Kihindi na tamaduni za Pwani. Eneo la mjini mkongwe bado lina peperusha bendera ya mji mkuu wa tamaduni za kiswahili.

**7. Kondoa michoro kwenye miamba**

Eneo hili lilitambulika kama eneo lenye urithi wa dunia hasa likiwa na umuhimu kihistoria kwa jamii za binadamu walioishi miaka 2000 iliyopita wenye asili ya uwindaji, mnamo mwaka 2006 likiwa katika wilayani Kondoa, mkoani Dodoma.

Michoro hiyo imetawanyika katika maeneo mengi yaliyokaribu na bonde la ufa, na kuwa na taarifa nyingi za kihistoria zinazohusu mabadiliko na maendeleo ya binadamu wa kipindi hicho walichotegemea zaidi uwindaji.

**Hitimisho**

Ukiacha maeneo mawili ambayo ni pori la akiba la Selous na magofu ya Kilwa Kisiwani kuwa maeneo yaliyo hatarini zaidi kuharibika na kupoteza sifa ya kuwa maeneo ya urithi wa dunia.

Bado kuna changamoto zinazokabili maeneo mengi na zisipotatuliwa kwa wakati idadi ya maeneo yaliyo hatarini kutoweka yataongezeka.

Changamoto hizo ni pamoja na uelewa mdogo na hafifu wa maeneo yenye urithi wa dunia kwa kundi kubwa la watu, watu wengi nchini kutokuwa na tabia ya kutembelea maeneo yaliyohifadhiwa.

Kuna ujangili, ungezeko kubwa la idadi ya watu, kuchora michoro kwenye baadhi ya majengo ikiwa ni tofauti na taratibu za uhifadhi wa majengo hayo, na ulinzi mdogo katika maeneo hayo. hivyo kuharibiwa na binadamu imekuwa rahisi sana na baadhi ya watu kutupa taka taka hovyo hivyo kutokuwa na mvuto

Kupitia changamoto hizo, serikali kwa ujumla wake kuanzia ofisi ya waziri mkuu idara ya mazingira, wizara ya maliasili na utalii, taasisi zote zinazohusika katika kusimamia maeneo haya ikiwemo Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Mamlaka ya Usimamizi wa wanyamapori (TAWA).

Hii ni kushirikisha wadau mbalimbali wa utalii na uhifadhi waunde vikundi maalumu vya kusimamia maeneo yenye urithi wa dunia ikiwemo katika upande wa mawasiliano, kuelimishaji jamii, utalii, wafuatiliaji wa ukiukaji sheria pamoja na ulinzi ili kuweza kuzitatua changamoto hizo mapema na kudumisha maliasili zote za nchi yetu na zile zenye urithi wa kidunia.

# SELENA GOMEZ AMKASIRIKIA TRUMP



LOS ANGELES, Marekani

**STAA wa muziki na filamu wa Marekani, Selena Gomez, ameeleza kusikitishwa na hatua ya Rais Donald Trump kuwashikilia wahamiaji haramu.**

Kwa mujibu wa ripoti, wahamiaji zaidi ya 1,000 wanashikiliwa, huku wengi wao wakiwa ni raia wa Mexico.

Selena (32), ambaye ana asili ya Mexico, alisema: "Poleni. Watu wangu wameshambuliwa, wakiwamo watoto. Sijui kwanini."

## BRUNO MARS JINO TU SASA


LOS ANGELES, Marekani

**MWANAMUZIKI mwenye jina kubwa, Bruno Mars, ameeleza kufurahishwa kwake na rekodi ya kibabe aliyoweka katika mtandao wa Spotify.**

Siku chache zilizopita, Mars aliweka rekodi ya kuwa msanii wa kwanza kusikilizwa mara milioni 150 ndani ya mwezi mmoja.

Katika ujumbe wake kwa mashabiki, aliwataka kuendelea kufuatilia ngoma zake, akitania kuwa anaweza kumaliza madeni aliyonayo kupitia mafanikio hayo.

## TEM AKACHA SHOO KIGALI



LAGOS, Nigeria

**SUPASTAA wa muziki wa Nigeria, Tems, amekiri kufuta shoo yake ya mjini Kigali, Rwanda, kutokana na kile kinachoendelea DRC.**

Temi, mshindi wa tuzo za Grammy, amefikia hatua hiyo kutokana na mgogoro unaoendelea kati ya mataifa hayo.

Awali, Tems alitarajiwa kuingia Rwanda kwa ajili ya shoo aliyotarajia kuifanya Machi 22, mwaka huu.





# BENFICA KUNA KITU MALACIA

MANCHESTER, England

**KLABU ya Benfica imeshindwa kukamilisha usajili wa beki wa Manchester United raia wa Uholanzi, Tyrell Malacia.**

Awali, yalikuwepo mazungumzo kati ya Man United na Benfica. Klabu hiyo ya Ureno ilitaka kumsajili kwa mkopo.

# GALATASARAY WANATAKA MTU




ANKARA, Uturuki

**KLABU ya Galatasaray imeanza harakati za kumsajili beki wa zamani wa Newcastle United, Kieran Trippier.**


Wakati huo huo, klabu za Ligi Kuu ya Italia, ikiwamo Napoli, nazo zimeonesha nia ya kumsajili Muingereza huyo.

## MILAN JICHO LIPO GIMENEZ

MILAN, Italia

**KLABU ya AC Milan iko kwenye hatua za kumsajili mpachikaji mabao wa kimataifa wa Mexico, Santiago Gimenez.**

Gimenez mwenye umri wa miaka 23, anakipiga Feyenoord na PSG nayo imeonesha nia ya kuinasa saini yake.



## MAN UNITED HESABU KWA TOURE

MANCHESTER, England

KLABU ya Manchester United imejitosa mazima katika harakati za kumsajili straika wa Mali, El Bilal Toure.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 23, kwa sasa anacheza kwa mkopo Stuttgart akitokea Atalanta.

BUSATI MICHEZO

Jumanne Februari 4, 2025 Tovuti: www.

# SIMBA YATOA TAMBO



NA ASHA SEKEFU

**UONGOZI wa Simba umeweka wazi kuwa umefurahi kulipa kisasi dhidi ya timu ambazo zilifungwa na Tabora United kwenye mechi za ushindani ambazo zilichezwa msimu wa 2024/25 ndani ya uwanja.**

Simba imecheza mechi 16 za Ligi Kuu Tanzania Bara inayodhaminiwa na NBC ikiwa ni ligi namba nne kwa ubora Afrika.

Timu hiyo inayonolewa na Kocha Mkuu, Fadlu Davids ni namba moja kwenye msimamo ikiwa na pointi 43 ikifuatiwa na Yanga yenye pointi 42.

Juzi baada ya dakika 90 ubao wa Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi ulisoma Tabora United 0-3 Simba kwa mabao ya Leonel Ateba ambaye alifunga mabao mawili dakika ya 12 na 33, huku bao moja likifungwa na Shomari Kapombe dakika ya 65 akitumia pasi ya Ateba.

Ateba kwenye mchezo huo alichaguliwa kuwa mchezaji bora wa mchezo kwa kuhusika kwenye mabao yote matatu yaliyofungwa na timu hiyo.


Akizingumzia mchezo huo, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally alisema kuwa wamelipa kisasi kwa timu zote za Dar es Salaam ambazo zilifungwa na Tabora United kwenye mechi za ligi ndani ya dakika 90.

# Man United kumbe hamna kitu

MANCHESTER, England

KIPIGO cha mabao 5-1 kutoka kwa Crystal Palace kimemuibua nahodha wa zamani wa Manchester United, Rio Ferdinand, ambaye ametoa kauli inayoweza kuwakatisha tamaa zaidi mashabiki wa klabu hiyo.

Man United, licha ya kuwa katika Uwanja wake wa nyumbani wa Old Trafford, iliendeleza mwenendo mbovu kwa kupoteza mchezo huo wa Ligi Kuu ya England (EPL) uliochezwa wikiendi iliyopita.



Akizungumia mchezo huo wa Jumapili, ambao ni wa tano kwa United kupoteza nyumbani, Ferdinand alisema kwa sasa hakuna timu inavyokwenda Old Trafford ikiwa na hofu ya kufungwa.

Mabao ya Palace yaliyofungwa na Jean-Philippe Mateta yameifanya Man United kushika nafasi ya 13 katika msimamo wa EPL.

"Kuna aliyeshangaa? Nafikiri hapo ndipo ilipofikia. Sijashangaa. Man United tumefungwa tena nyumbani leo. Timu zinazokwenda Old Trafford kwa sasa hazina cha kuhofia," alisema.

Kwa upande mwingine, Ferdinand alisema kocha wa Man United, Ruben Amorim, ana kazi kubwa.